

Mungu Zaidi Ya Kamusi Yetu (God Beyond Our Dictionary)

Na

John Kombo

Mungu Zaidi Ya Kamusi Yetu (God Beyond Our Dictionary)

Na

John Kombo

March 18, 2014

Mungu Zaidi Ya Kamusi Yetu

Kama tulimuumba Mungu tungeelewa, hivyo, nidhahiri tunaweza kuingiza katika akili zetu shauku kuhusu uwepo wake. Kama tunapaswa kumwamini Mungu, bila shaka Mungu huyu ni lazima azidi uelewa wetu.

Mungu wa kweli yuko zaidi ya fikra zetu. Ni zaidi ya uelewa wetu kamili ni kwa sababu yeye ni Mungu; na sisi ni wanadamu.

Mungu anakuja kwa mwanadamu kwa mawazo ya kimbingu ambayo pia iko zaidi ya uelewa wetu kwamba tunadaiwa na kusenkenya katika uwezekano wake, tunasenkenya katika ualisia wake; tunapiga miayo kwa uwepo wake. Hataivyo, ni kwa sababu iko zaidi ya uelewa wetu, tunaweza kutilia shaka uwepo wake.

Muumba ni lazima awe mkuu kuliko kiumbe.

Roho Mtakatifu huja kwetu na kitabu cha maneno ya wanadamu, Biblia. Tunapaswa kutambua kwanza kwamba hakuleta kamusi ya kimbingu.

Pale alijifunza hili pale alipokutwa katika Paradiso na kusikia *“maneno yasiyoelezeka,...ambayo haikuwa sheria hata kutamkwa.”* (2 Kor. 12:1-4). Hazikuwa sheria kunenwa kwa sababu hatuna kamusi ya kimbingu ambayo inatafsiri sambamba zaidi ya ulimwengu wa uelewa wetu.

Hivyo, alikuja kwetu katika Biblia kwa sitiari. Kitabu chake kilichovuviwa kimejaa sitiari kama, *“uso wa Mungu” “mitaa ya dhahabu”* na *“moto uwakao kwa kiberiti”*

Mungu anawasiliana nini? Tunaweza kufahamu kwamba sitiari hisi hutuonyesha kitu kikubwa kuliko sitiari, kuu kuliko tafsiri ya ulimwengu?

Katika mshituko wetu wa kumuelewa Mungu, kimbilio letu la kwanza ni kumuumba Mungu kwa sura zetu. Tunamtazama Mungu kama sisi wenyewe, kwa uwepo wetu wa kimwili. Tunahitimisha kwamba Mungu anamkono halisi; ana uso halisi, macho, masikio, na maneno ya sauti. Alafu tunachora sura yake katika makaratasi kwa kutumia kalamu na mikono yetu.

Katika mazingira yetu ya kitoto tumemleta Mungu chini hadi tutakapomuelewa. Sasa ametoka katika Mungu hadi katika miungu.

John Kombo Nandwa

Nakuru, Kenya

